**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU**

**Simu Na.** **+255 752 663 188**
**+255 621 288 371**
**+255 766 268 822**
**Email:** kishapusek@gmail.com

Shule ya Sekondari Kishapu
S.L.P 1240
**SHINYANGA.**
26/04/2024

Kumb. Na.: KSS/JN/KIDT 5/VOL I/2024/01
**Mzazi/ Mlezi wa: …………………………………….**
**S.L.P ………………………………………………….**
**……………………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISHAPU WILAYA YA KISHAPU MKOA WA SHINYANGA MWAKA 2024**

## 1. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga Kidato cha Tano (V) katika shule hii mwaka 2024, tahasusi ya________. Shule ya Sekondari Kishapu ipo umbali takribani kilometa 56 mashariki mwa mji wa Shinyanga. Ukifika mkoani Shinyanga uliza soko kuu la mkoa, hapo utapata Daladala zitakazo kuleta Wilaya ya Kishapu Mji wa Mhunze. Kutoka Shinyanga mjini hadi wilayani Kishapu mjini Mhunze nauli ni Tshs. 4,000/= na Tshs. 1,000/= utalipia Bodaboda, ambapo utafikishwa hapa Shuleni.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **01.07.2024**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe Kuanzia **29.06.2024** na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe **15.07.2024.**

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### A. Sare ya Shule

**Vifaa na sare za shule zinapatikana shuleni au unaweza ukajishonea /kununua nyumbani**

**(i) Wavulana**

(a) Suruali mbili (2) rangi ya ***Damu ya Mzee*** za kutumia darasani mfano wa kitambaa umeambatanishwa , suruali hizo ziwe na malinda mawili tu , iwe na SM 16 na sio pungufu pia Suruali mbili (02) **Rangi Nyeusi** (shamba dress) ziwe na malinda mawili tu , iwe na SM 16 na sio pungufu

***Muhimu:*** **SIKU YA KURIPOTI MWANAFUNZI AJE AKIWA AMEVAA TRAKI SUTI RANGI YA BLUU NA SIO VINGINEVYO.**

(b) Mashati mawili meupe mikono mifupi yasiyo na urembo wowote na yenye mfuko mmoja upande wa kushoto.

(c) Fulana (T- Shirt) mbili. Hizi zitapatikana shuleni @ Tshs. 12,000/= tu.
(d) Viatu vya Ngozi vyeusi vilivyo na Gidamu na kisigino kifupi (Sio buti) (Jozi mbili).
(e) Chandarua 1 kwa ajili ya mbu iwe ya bluu.
(f) Soksi nyeusi ndefu (Jozi mbili)
(g) Mkanda mweusi wa Ngozi (Kwa ajili ya Kuvalia suruali) usiwe mpana na usiwe na kichwa chenye sanamu au urembo wa aina yoyote, na usiwe utambi.
(h) Godoro lenye futi 2.5×6
**(i)** Mto, Shuka mbili na foronya mbili **Rangi ya bluu bahari**
**(j)** Vifaa vya michezo kama vile Bukta, jezi, traki suti (Zote ziwe za rangi ya Bluu), raba/ viatu vya mpira .**Ambazo sio Jezi za timu yeyote / zisiwe na logo/nembo/ jina la timu yeyote..**
(k) Sweta rangi Nyekundu (Damu ya mzee).
(l) Blanketi moja (1) rangi ya bluu bahari .
(m) Tai ndefu rangi sawa na suruali ya shule
**(n) ZINGATIA: KWA MWANAFUNZI ALIYEKUWA MWANACHAMA WA SKAUTI NA ANAPENDA KUENDELEA NA SKAUTI AJE NA SARE ZA SKAUTI.**

**(i) Mahitaji Muhimu ambayo Mwanafunzi anapaswa kuleta Shuleni ni;**

a. Ream ya Karatasi (A4) mbili (2) kwa Mwaka. Zinaletwa kwa awamu moja anaporipoti.
b. Vitabu vya Masomo husika. MZAZI UNASHAURIWA UMNUNULIE MWANAO VITABU.
c. Counter Books Nane (8) na Faili mbili.
d. Scientific Calculator 1
e. Daftari ndogo Kumi (10)
f. Kalamu za Kuandikia (Pen) ya bluu au nyeusi, penseli na mfuto.
g. Mkebe mmoja/ Mathematical Set 1 na Rula ndefu 1.
h. Vyombo vya Chakula (Sahani, Bakuli, Kijiko, na Kikombe)
i. NDOO mbili (2) ndogo zenye mfuniko.
j. Kwanja 1, panga 1, Jembe 1 (lenye Mpini), Mfagio wa ndani (Soft Broom) 1, Mfagio mgumu (Hard Broom) 1 na Mopa 1.

**ANGALIZO**: ***Hatupokei fedha Mkononi kwa ajili ya manunuzi ya mahitaji tajwa hapo juu, mwanafunzi aripoti akiwa na vifaa hivyo.***

**B. MICHANGO MBALIMBALI**

Pamoja na mahitaji muhimu ya shule, mwanafunzi anapaswa kuchangia shule mahitaji yafuatayo ili kuboresha ufanisi wa shule;

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo ya Shule | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| **Jumla** | | **80,000/=** |

**C. BIMA YA AFYA**

**Kila mzazi / mlezi amkatie mwanae Bima ya NHIF ya Tsh 50,400 /= kwa mwaka au alipe shuleni kiasi cha Tsh 50,400 /= kwa ajili ya bima hiyo . kwa mwanafunzi ambaye tayari ana bima ya NHIF aje nayo na mchango wa Tsh 50,400 /= hautamhusu.**

**Malipo yote yafanyike Benki isipokuwa sare za shule, kupitia akaunti ya shule ambayo ni;**

***Jina la Benki*: NATIONAL MICROFINANCE BANK (NMB)**
***Namba ya Akaunti*: 30701100044**
***Jina la Akaunti*: KISHAPU SECONDARY SCHOOL- RECCURENT**

**MUHIMU**

1. **Tafadhali hakikisha unaandika Jina la Mwanafunzi kwenye hati ya malipo ya Benki yaani *Pay slip***
2. **Malipo ya sare za shule (Angalia kipengere namba 2, A(i)) yasiwekwe kwenye akaunti ya shule tajwa hapo juu, Mwanafunzi aripoti akiwa na fedha tu, mahitaji atayakuta shuleni.**

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

(a) **Heshima** kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni **lazima**.
(c) Kushiriki kwa makini Maandalio ya jioni (**Preparation**) kwa wanafunzi wa Bweni.
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
(h) Kutunza mali za umma.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na SIMU shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye BWENI alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (MSIBA AU UGONJWA).**

**Makosa Yanayoweza Kusababisha Kufukuzwa na Kusimamishwa Shule ni;**

(a) Wizi.
(b) Kutohudhuria Masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa (Utoro).
(c) Uasherati, Ulawiti, Usagaji na Ushoga.
(d) Ubakaji.
(e) Kufuga Ndevu.
(f) Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzako, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
(g) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji **Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli**, na kadhalika.
(h) Kupiga au Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kupigana na mwalimu au mtu yeyote yule.
(i) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(j) Kudharau Wimbo na Bendera ya Taifa.
(k) Kusababisha Mimba, kumpa Ujauzito Msichana.
(l) Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(m) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(n) Kuoa.
(o) Kuwa nje ya eneo la shule bila ruhusa.
(p) Kugoma, kuhamasisha mgomo, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(q) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(r) Kuwa na **SIMU** ya mkononi, **CAMERA, REDIO** na vitu vingine vyote vya kufanana na hivyo.

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU**

# FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

**Anuani ya Mzazi/ Mlezi**
**…………………………………………….**
**…………………………………………….**
Tarehe**: ……………………..**

**Kumb. Na. KSS/JN/KIDT 5/VOL 1/2024/02**
SHULE YA SEKONDARI KISHAPU
S.L.P 1240
**SHINYANGA.**

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISHAPU**

**A. MWANAFUNZI**

1. Mimi (Jina la Mwanafunzi) ……………………………….............. (Herufi Kubwa), nimepokea, nimesoma na nimeelewa vizuri Masharti/ maelekezo ya kujiunga na masomo ya Sekondari Kidato cha TANO katika Shule ya Sekondari Kishapu mwaka 2023. Na ninakubali kujiunga na Jumuiya ya Shule ya Sekondari Kishapu, ninaahidi kutoshiriki katika Migomo, Fujo na Makosa ya jinai, nitakuwa mtiifu nitazingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za shule kama nitakavyoelekezwa.
2. Ninaahidi kwamba nitazitii Sheria za Shule na kuwahi kurudi Shuleni kila baada ya likizo bila kuchelewa.
3. Nitahudhuria katika vipindi vya masomo yote ikiwa ni pamoja na vipindi vya dini na kuyafanya Mazoezi na mitihani yote kama itakavyopangwa.
4. Nitashiriki katika shughuli za Elimu kujitegemea, michezo, na usafi wa mazingira ya shule.
5. Nitakuwa nawasiliana na walimu pamoja na wanafunzi wenzangu kwa kutumia lugha ya kiingereza wakati wote.

***Sahihi ya Mwanafunzi***: …………………………………… ***Tarehe***: …………………………..

**Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi**
Jina:______________________________
Saini:_____________________________
Tarehe: ___________________________

©KSS072024

**KIAMBATANISHO B**

***(Karatasi hii Lazima irudishwe Shuleni ikiwa imejazwa)***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU**

**Simu Na.** **+255 752 663 188**
**+255 621 288 371**
**+255 766 268 822**
**Email:** kishapuss@gmail.com

Shule ya Sekondari Kishapu
S.L.P 1240
**SHINYANGA.**

Tarehe: ________________

Kumb. Na.: KSS/JN/KIDT 5/VOL I/2024/03
**Ndugu Mzazi/ Mlezi wa: ___________________________________**

## MKATABA WA KUMSOMESHA MWANAO____________________________

1. JINA LA MZAZI/MLEZI *(kata moja)* ____________________________________________
   Naahidi kumtekelezea mahitaji yake yote mwanangu ______________________________ kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa, na nitashirikiana na Uongozi wa Shule katika kumlea kijana huyu, ili kuweza kufikia lengo la Elimu la Taifa.

2. Nitahakikisha anawahi kurudi Shuleni kila baada ya likizo.

3. Wafuatao ni ndugu/ Rafiki zangu wa karibu wanaoweza kunisaidia kama kuna dharura ***(Njoo na picha zao za Passport)***

| | JINA LA NDUGU | UHUSIANO | ANUANI YAKE | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| (i) | ______________________ | _____________ | __________________ | ________________ |
| **(ii)** | ______________________ | _____________ | __________________ | ________________ |
| **(iii)** | ______________________ | _____________ | __________________ | ________________ |
| **(iv)** | ______________________ | _____________ | __________________ | ________________ |

4. Ripoti za maendeleo yake kutoka shuleni ziwe zinatumwa kwa ______________________ (Taja Jina) mwenye anuani ifuatayo __________________________________

5. Mwanangu ni muumini wa Dini:_______________Dhehebu la _________________________

6. Namba yangu ya simu kwa mawasiliano ya haraka ni ______________________

**Saini ya Mzazi/ Mlezi**
________________________________

**Namba ya Simu ya Mzazi/ Mlezi**
___________________________________

**Tarehe**
______________________

**KIAMBATANISHO C**

*(Karatasi hii Lazima irudishwe Shuleni ikiwa imejazwa)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

**A. MWANAFUNZI**

(i) Jina la Kwanza:________________________________________________________
(ii) Jina la Kati:__________________________________________________________
**(iii)** Jina la Ukoo:_________________________________________________________
(**Majina haya lazima yabaki hivihivi kwa miaka yote uwapo shuleni Vinginevyo ulete Kiapo cha mahakama kinachoonesha umebadili jina)**
(iv) Tarehe ya Kuzaliwa: ……………………………………………………………….
(v) Mahali ulipozaliwa:
Wilaya: ……………………………… Mkoa: …………………………………….
(vi) Dini: ………………………………. Dhehebu: ………………………………….
(vii) Shule uliyomaliza Kidato cha Nne (IV): …………………………………………...
(viii) Je uliwahi kuwa Kiongozi (Kiranja) ……………………………………………….
(ix) Kama jibu hapo juu (viii) ni ndio, taja wadhifa/ Cheo ……………………………..
(x) Je katika Ukoo wako kuna magonjwa ya kurithi? (Ndiyo/ Hapana) Yataje
……………………………………………………………………………………….

**B. BABA**

(i) Jina la Baba yako: ………………………………………………………………..
(ii) Yu hai? NDIYO/ HAPANA: ……………………………………………………….
(iii) Kama amefariki taja tarehe: ……………………………………………………...
(iv) Anuani yake: ……………………………………………………………………..
(v) Namba ya Simu: ………………………………………………………………….
(vi) Kazi/ Cheo chake: ………………………………………………………………..
(vii) Dini ya Baba yako: ……………………... Dhehebu: ………………………………

**C. MAMA**

(i) Jina la Mama yako: ………………………………………………………………..
(ii) Yu hai? NDIYO/ HAPANA: ……………………………………………………….
(iii) Kama amefariki taja tarehe: ……………………………………………………...
(iv) Anuani yake: ……………………………………………………………………..
(v) Namba ya Simu: ………………………………………………………………….
(vi) Kazi/ Cheo chake: ………………………………………………………………..
(vii) Dini ya Mama yako: ……………………... Dhehebu: ……………………………..

**D. MLEZI**

Mlezi ni mtu asiye Mzazi wako anayekutunza na kukuhudumia kwa chakula, malazi na mavazi.

(i) Jina la Mlezi wako: …………………………………….Jinsia (Me/Ke): …………
(ii) Uhusiano wako na Mlezi ni (Mjomba/Kaka/Rafiki/Shangazi/ n.k): …………………
(iii) Anuani ya Mlezi wako: …………………………………………………………
(iv) Kazi ya Mlezi wako: ……………………………………………………………
(v) Anaishi kitongoji gani? ……………………… Kata ya …………………………….
(vi) Jina la Mwenyekiti wa Kitongoji: ……………………………. Simu: ……………….
(vii) Jina la mtu atakayepelekewa ripoti za shule ………………………………………..
Anuani: …………………………………. Saini: …………….. Simu: ………………………..
Uhusiano: ………………………

Ninakiri kuwa maelezo yote yaliyoandikwa hapo juu ni sahihi na ni ya kweli.
Saini ya Mwanafunzi: ………………….. Tarehe: ……………………
Jina la Mzazi/ Mlezi: ………………………………….Saini ya Mzazi/Mlezi: ………….. Tarehe: ……………

**ORODHA YA VITABU KWA KILA TAHASUSI (COMBINATION)**

**GEOGRAPHY BOOKS:**

1. **Mcknight, T, (2008), Physical Geography A l and scape appreciation, prentice Hall USA.**
2. **Bunnet, R. (1973), General Geeography in Diagram, Education Singapore**
3. **Pritchard, J, (1984) Practical Geography in diagram, Education Singapore**
4. **Morgan – human economic geography**

**HISTORY BOOKS:**

1. **Longman – history – new version**
2. **Shibital – history one and two**
3. **Advanced level history paper one and two by Zisti kamili**
4. **History form 5 and 6 by scu and MOEVT – Zanzibar**

**ENGLISH LANGUAGE**

1. **Advanced dictionary of contemporary English**
2. **Apractical approach 2$^{ND}$ edition – Nicholaus Ashel**
3. **Writing skills – Kiura**
4. **Contemporary English for Advanced Level (Form 5&6), The Competence Based Approach 3$^{rd}$ Ed. – Francis Mnyawi.**

**ECONOMICS**

1. **Modern economic by dr Dewit**
2. **Modern economic by Robert Pandic**
3. **Principle of economic by Jinghan**
4. **Simplified economic by saalem**

**GENERAL STUDY**

1. **Johnnes Bigirwamungu and Sospeter m.Deogratius understanding general studies for advanced level**
2. **Nyambari nyangwine contemporary approach for advanced level general studies notes.**

**NB: Kila mwanafunzi anashauriwa anunue kitabu angalau kimoja kwa kila somo.**

## E. HITIMISHO

Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Napenda tena kutumia fursa hii kukupongeza kwa kupata nafasi hii adimu ya kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano (V) hapa Shule ya Sekondari Kishapu. Ni matumaini yangu hautaiacha nafasi hii Muhimu kwako ipotee bure.

**MUHIMU:**

**KUUNGANISHWA KWENYE GROUP LA WHATSAPP LA WAZAZI WA WANAFUNZI KIDATO CHA TANO 2024 /2025 KISHAPU SEKONDARI WASILIANA NA 0621 288 371. PIA KUNDI HILI LITATUMIKA KUTUMA MATOKEO YA MITIHANI ATAKAYOFANYA MWANAO HAPA SHULENI.**

**Hongera sana na Karibu Shule ya Sekondari Kishapu.**

**BUHORO NG'WANDU MIPAWA**
MKUU WA SHULE

**NB:**
Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/ MTOTO WAKO USITUME FEDHA YOYOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule **0752 663 188**
- Makamu Mkuu wa Shule **- 0628 947776**
- Mwandamizi Taaluma **0621 288 371**
- Mwandamizi Malezi **0783 675 055**

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

## KISHAPU SECONDARY SCHOOL
## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**DATE: ………………….**

**PART A.**

Mr/ Miss …………………………………………………………………

Please, Examine the above-named person, his/ her Physical and Mental fitness for a full-time learning.

The examination should include the following categories: -

1. Eye
   Hearing
   Limbs
   Speech
   General Disease
   Leprosy
   Epilepsy

2. Neuroses
3. Other serious diseases
4. Pregnancy

**PART B.**

(To be completed by Government Medical Officer) I have examined the above-named person and consider that HIS/ HER is Physically *Fit/ Unfit and Mentally *Fit/ Unfit for full time learning.

1. Eye ……………………………………………………
   Hearing ……………………………………………………
   Limbs ……………………………………………………
   Speech ……………………………………………………
   General Disease ……………………………………………………
   Leprosy ……………………………………………………
   Epilepsy ……………………………………………………

2. Neuroses ……………………………………………………
3. Other serious diseases ……………………………………………………
4. Pregnancy …………………………………………………….

SIGNATURE: …………………………Stamp: …………………… DATE: …………………



